Isaya Joe ni mwanaume nani mume niliyempenda sana kuliko wanaume wote ulimwenguni.
Upendo wetu ulianza toka tukiwa vijana wadogo na wanafunzi wa shule ya msingi mtamani.

Baada ya kumaliza darasa la Saba matokeo haya kua mazuri kwa upande wangu, kwakua haya kuniwezesha kuendelea na elimu ya secondari.

Isaya alifanya vyema ila alishindwa kuendelea na kidato cha kwanza kutokana na umasikini uliokua umetawala ndani ya familia yake.

Baada ya miezi kazaa baada ya matokeo kutoka, Isaya alifanikiwa kupata nafasi ya kwenda kupata mafunzo ya jeshi jijini dar es salama, na kuniacha kijijini Mkia ndege akiniahidi anakwenda kutafuta maisha, ata rejea kwa ajili yangu.

Nilimuahidi kumtunzia usichana wangu mpaka atakapo rejea kijijini mkia ndenge ata ikimchukua miaka ishirini, ni tamsubiri tuh!.
Niliamini mafanikio yake ndio mafanikio yangu, na kuamua kumluhusu kwa roho nyeupe.

Miaka miwili toka Isaya kuondoka kijijini Mkia Ndenge, wanaume wengi walikuja
nyumbani kunichumbia matajiri kwa masikini.

Nilizikataa posa zote kwakua sikua tayali kuivunja ahadi niliyompatia kijana Isaya japo muda ulipita sana bila hata ya barua ya salamu, nilijipa moyo siku moja hata rejea kwangu.

Jambo lililonifanya nionekane watofauti kijijini hasa kwa wasichana warika kama langu walio kuwa wanandoto za kuwahi kuolewa, wengi waliona na ikimbia bahati.

Wengine walininyoshea vidole nilipo pita karibu nao na kusema.

Chakulinga huyo anaejiisi yeye ni mzuri sana, kiasi cha kukataa kila mwanaume anae kuja kumchumbia hapa Mkia Ndege

Huyu mchagua nazi ipo siku ata pata koloma tupo hapa

Maneno ayo japo yalikua ya na choma na kukera nafsi, kamwe haya kuweza kubadili kitu
moyoni mwangu.

Ilikua kawaida kwangu kila jioni ifikapo kwenda kisimani kuchota maji ya kuoga,
Siku moja ni kiwa natoka kisimani njiani nilisikia sauti ya mwanaume ikiniita.

Imerida! Imerida!

Edit with WPS Office

Sauti hiyo ikitokea kichagani niligeuka na kutazama uku na kule ila siku muona mtu.
Kwa hofu niliongeza mwendo wa kutembeaa.

Nilipo piga hatua chache ghafla walitokea vijana wengine watatu mbele yangu wakitokea
vikichakani mikononi wakiwa na vidumu vya lita tano kila moja.
Kwa sauti ya hofu niliwauliza

Jamani mwataka nini kwani

Ahaahaha wewe si bingwa wa kukataa wanaume hapa kijijini sasa leo tutakuonyesha sisi ni wakina nani na tutaona baada ya hapo ni nani atakae kuoa hahaha

Leo ndio utakua mwisho wako wa kutulingia hapa kijijini alaaaa

Nilipo mgeukia kijana yule aliye niita kwanza na kumuomba anisaaidie ila jibu la kijana huyo lilinimaliza nguvu kabisa

Wewe si unatuzarau wanaume wa kijiji hiki basi wacha leo tukuonyeshe faida ya mtaji wako ulio ekeza mioyoni mwetu sawa malikia wa mtamani

Niliingiwa na hofu ali iliyopelekea mpaka kuangusha ndoo.

"Jamani msinifanyie chochote na waomba" ila ombi langu alikuasaidia kitu walinisogelea waliponi Karibia walini beba kama mzoga na kutokomea vichakani.

Nilijaribu kupiga kelele ili nipate ata msaada ila aikusaidia kitu kwa kua kisima kilikua maeneo ya mashambani mbali na makazi ya watu.

Walipoona na piga kelele sana walichukua kanga niliyo kua nimejifunga ngata kichwani na kunifunga mdomo.

Walinitendea unyama wa kunibaka na kutokomea vichakani, nilihisi maumivu makali sana huku damu zikinitililika kama maji ya shukavyo kwenye maporomoko.

Niliamua kujikongoja ni kiwa natumani ni kimaliza eneo la mashamba nitapata msaada kwa wanakijiji, ila ali ilikua tofauti sana baada ya msaada nilipata zihaka nilipo anza kuingia mwanzo wa makazi ya watu kijijini.

nilijua akuna msaada kila nilipoinua nyuso yangu na kuwatazama kwa uso wa huruma ila wengi wao walikua wakinicheka tu,wakimaanisha tendo nililifanyiwa wamefurahishwa nalo na walikua wa naomba siku moja linitoke.

Aya sasa malikia wa kijiji kafanywa kua chaote ahaha,

Edit with WPS Office

Bora walivyombaka tu jamani, maana tulikua atunywi ata maji hapa kijijini kwa ajili yake

ninani aliye jiolea malikia wetu wa kijiji bila ya mshenga wala barua hahaha, mtafuteni
nimlipe ata magunia mia ya ufuta akauze pate ata ela ya pombe

Walizungumza mengi sana.

Maneno yao yalinifanya nijisikie aibu sana, jambo lililo nifanya ni jitaidi kutembea maana nilitambua kwa wakati huo msaada pekee ni nyumbani kwa wazazi wangu.

Nilipo fika nyumbani mama alishangaa alipoliona gauni nililo vaa limechanika chanika na damu zikini mwagika misili ya mvua ya masika.

Jamani mwanangu nini tena, mkosi gani huu katika familia yangu
Nilibakia tu kulia

Mama naumia mama nimebakwa mimi….. naumia mama….. naumia mwanao
Kauli ile ilikua ya mwisho kimywani mwangu nilianguka na kupoteza fahamu.

Nilipo kuja kushituka nilijikuta nipo kwenye kitanda na mwilini ni kiwa na vazi jeupe pembeni yangu alikua mama akitokwa tu na machozi uku akiwa amejiinamia.

Niliita mama, mama alishtuka
"mwanagu imerida"
alinitazama uku machozi ya kimtoka kwa kasi Nilishanga mama Analia kwa sababu gani na kwanini nipo maeneo hayo.

Nilipo jaribu kuinuka ilinimpanguse mama machozi nilihisi maumivu makali mwilini kuanzia maeneo ya kiunoni kwenda chini hapo kumbukumbu za kubakwa ziliniludi na baada ya kumbembeleza mama mwishoe tulijikuta tuna lia wote.

Nyamaza mwanangu nyamaza mtoto wangu ndo changamoto za maisha

Mama Usichana wangu ….!Mama kwa nini awakuniua kwani….nimewakosea nini mimi kukataa kuolewanao ni kosa kubwa sana et mama..?

mama alibaki tuakinipigapiga mgongoni
Nilipiga sana mayoe mule chumbani jambo lililowafanya madaktari wa liokuwa zamu waje na kunichoma sindano ya usingizi.
Maisha ayo ya sindano niliishi nayo takrbani miezi mitatu siku weza kujizuia kila nilipo amka na kulikumbuka tukio ilo nilibaki tu nikipiga mayowe ya uchungu kama chizi.

Edit with WPS Office

Familia yangu ilipata wakati mgumu sana ndani ya jamii kwa kuchekwa, kutukanwa na ata kutupiwa mawe na makopo yaliyo kuwa na mikojo ndani yake, wakiitwa familia ya kizazi cha laana.
Baada ya miezi mitatu kupita hatimaye niliruhusiwa kurudi nyumbani, bado ni kiwa chini ya uwangalizi wa madaktari.
Sikutamani kuludi kwenye kijiji kile niliona kama shimo la moto kwangu na kwa familia yangu ila sikua na sehemu ya kwenda zaidi ya kijijini mkia ndege.

Baada ya wiki kazaa kupita toka nileje nyumbani, siku moja asubuhi mlango wa chumba changu
uligongwa….ukisindikizwa na sauti ya mama

imerida mwanangu usha amka mama..?

kwa muda huo nilikuwa nisha amka nimeketi kitandani.

Usijali wewe pita tu mama, Tena bora uje unisaidie kuni valisha nguo

Basi baada ya kutamka maneno ayo mama alifungua mlango na kuingia ndani moja kwa moja.
Baada ya salamu mama aliniuliza maswali ma wili matatu juu ya afya yangu ninavyo jisikia mwilini mama alini vishanguo na kunieleza kuna mgeni kaja kukuona.

Nilishanga sana kwa kua ilikua asubuhi sana pia toka nitoke hospitali akuna mwana kijiji yoyote aliye wahi kuja kunijulia ali zidi tu ya kuniombea mambaya juu yangu na familia yangu kila kulipo itwa leo.

Mgeni....! Mgeni gani tena asubuhi…yote hii.

Wakiume ama wakike

wakiume mwanangu, tena ndo mara ya kwanza kumuona

Mh aya twende tuka muone

Basi sikutaka kuendelea kumuliza mama, na kumuomba anisaidie kunyanyuka ili tutoke tukamuone huyo mgeni.

Mama alinisaidia kunitoa mpaka nje, akika sikuamini kile nilichokiona machoni mwangu nilihisi mwili mzima na tokwa na majasho uku viungo viki legea na kushindwa ata kupiga tena nusu atua, machozi ya kinibubujika nilimuomba mama ni kae chini kwanza mama alinikalisha.

Uso wa mama ukiwa na mshangao, macho yake ya kipata shida kututazama wote wawili kwa wakati moja.

Isaya Joe ni wewe ama bado nipo usingizini mama et eh?

Edit with WPS Office

Nilimuliza mama maana siku amini kweli ni isaya mwanaume ninae mpenda kupita wote
ulimwenguni niliyemsubili takribani miaka miwili leo hii yupo mbele ya macho yangu.

Imerida zigamba..! Mwanamke wangu wa maisha

Sauti ya isaya iliniita uku akionyesha tabasamu usoni mwake na akipiga atua akisogea pale chini nilipo keti.

Isaya alipo fika pale chini nilipo keti ali inama nakupiga magoti, mama aliamua kutuacha wawili na kuelekea jikoni
.
Imerida mke wangu isaya aliniita

Sikuwa na ujasili wa kuitikia niliona aibu ndani ya moyo wangu niliona astaili kuniita mke angali sina usichana tena nilio muaidi nita mtunzia.

Tena ukizurumiwa kwa kitendo cha aibu katika jamii….na kubaki kimya uso wangu ukitazama ardhini pasipo kumtaza Isaya usoni.

Mbona uniangali mama angu

Naomba uniache isaya na uwende zako, sifai tena kua mkeo sifai isaya

Baada ya kauli hiyo nili baki ni kibubu jikwa na machozi.

Imerida...Zig...

Isaya kabla ya kumaliza kulitaja jina langu nilimkatisha kwa maneno ya uchungu kinywani Mwangu.

Samahani Isaya, mama naomba uje uni rudishe ndani

Mama Alikuja, na kunibeba akanirudisha ndani nilimwacha isaya akiita tuh

Imerida…..naomba unisikilize….naomba emerida

Moyoni mwangu nilijiisi naungua kila nilipo geuza shingo na kumuona isaya pale chini.
Kwakua ni mwanaume niliye mpenda sana kuliko kitu chochote.

Nilipofika ndani mama alinishusha kitandani na kunieleza

Msikilize mwenzako mwanangu

Mama sina ujasili wa kuongea na isaya mama nampenda sana, mama huyu ndo mwanaume niliye kua ni kimsubilia miaka yote, Kwanini Kachelewa kwanini mama! Unazani haya yote yaliyo ni kuta bado tuh ata baki

Edit with WPS Office

kunichukulia kama mwanamke wakipeke kwake, usichana wangu niliomuahidi nitamtunzia uko wapi mama, Mama na jiogopa, na uogopa ata huu mwili nilionao.

Mama alibaki kimya na kunikumbatia tu kwa uchungu.

Alinibembeleza mpaka ni kalala alitoka na kuniacha kitandani.

Mchana wa siku hiyo uligubikwa na huzuni na maumivu ya moyo ata chakula kilishindwa kupita kooni na kuomba wa niache peke yangu chumbani.

Usiku ulipo ingia mzee zizi wa zigamba alirejea nyumbani akitokea kwenye mizunguko yake ya maisha, baada ya chakula cha usiku baba aliniomba ni bakie sebureni, kuna jambo anataka kunieleza, alitoka nje alipiga mswaki na kurejea sebureni na kuketi.

Mwanangu emerida mzee zizi wa zigamba aliniita.

Abee..! Baba

Kuna jambo nililieka moyoni kwa kipindi chote ulicho ugua mpaka leo sikuku eleza wewe wala mama yako,ila leo naomba ni waeleze sawa mwanangu

Ndio baba, nakusikiliza

Siku mbili baada ya tukio lako ulilofanyiwa na kupelekwa hospital, baba yako niliishiwa pesa kabisa ya kukununulia ata maji ya kunywa hosptali.siku iyo katika pita pita kijijini ni kiangaika angaika uku na kule kutafuta chochote kitu,kuna kijana nilikutananae na kunieleza amesikia tukio lililo kukuta na baada ya stori za hapa na pale kijana yule alingia mfukoni na kuni kabizi milioni moja na nusu na kunieleza.

Hii itawasaidia kwenye matibabu na kukiwa na tatizo lolote basi naomba tukutane hapa siku mbili mbele

Basi toka hapo kijana huyo alikua aki gharamikia matibabu yako kuanzia kula na vitu vingine vya msingi miezi yote ulio kaa hopstali mpaka leo hii.

Kijana mwenyewe anaitwa nani baba

Akutaka kutaja jina lake na kwakua muda huo mimi nilicho kua na itaji ni uzima wako, sikujali juu ya jina lake.ila kesho alinieleza atakuja asubuhi. baba alinijibu

Mhmh! sawa baba

Basi kesho ujue tuna ugeni asubuhi na mapema

Baada ya maneno hayo ya baba aliniruhusu kwenda kulala.

Edit with WPS Office

.
Kitandani usingizi ulikua auji kabisa uku ni kijiuliza ata kua isaya nini ila mwishoe nilijipa moyo angekua isaya mbona akuja kuniona hospitali kwa kipindi chote pia kwa nini akulitaja jina lake kwa baba na kitendo cha aibu nilicho fanyiwa iweje bado tuh aendelee kunisaidia maswali hayo yalinifanya kujipa moyo zaidi kua kijana huyo mwema kamwe sio isaya.

Asubuhi ilipofika mama aliniandalia maji ya kuoga nilienda oga,ni kavaa vyema gauni langu lefu nililo kua na pendaga sana kuvaa siku za jumapili kanisani.
Baada ya maandalizi yote nilielekea sebureni, nilimkuta baba akisoma gazeti na mama akifuma zake mkeka.

Niliwasalimu na kuketi kwa dhumuni la kuwasubili wageni.

Mama Alinieleza "ebu andaa chai kwa ajili ya wageni ni shaibandika kule jikoni

Nilishituka wageni kwani wa nakuja wa ngapi baba

Sijajua kwa kweli mwanangu ila alinieleza ata kuja na wazazi wake kututembelea
Baba alipo nijibu niliinuka nilipo keti na kuelekea jikoni.

Kama nusu saa hivi ilipita Mimi ni kiwa bado nipo jikoni naendelea na maandalizi ya chai na vitafunwa, nilisikia sauti ya mama ikiwa karibisha wageni hao walio kuja na kijana kwa dhumuni la kuja kuniona.

Baada ya salamu na stori za hapa na pale mama aliniita ni peleke chai sebureni.
Nilianda vyema chai na kuanza safari ya kwelekea sebureni, nilipo fika sebureni siku amini kama kijana aliye ni saidia muda wote ni Isaya Joe na leo amekuja kwetu akiambatana na wazazi wake.

Nilijikuta tu nikitamka isaya ni wewe tenah

Watu wote sebureni walishtuka na kuuliza kumbe mnajuana? mama aliposikia jina ilo alinigeukia na kuniuliza ni kijana huyu ndie aliye kuja jana asubuhi.

Ndio mama ni mimi isaya alijibu

Ebu njoo hapa uketi

Baba alinieleza nilisogea uku macho yangu yote ya kimtazama isaya na kuketi karibu na baba yangu mzee zizi wa zigamba.

Mnafahamiana wewe na huyu kijana baba aliuliza

Edit with WPS Office

Kabla sija jibu isaya alimjibu baba
Mimi na binti yako tumeanza kufahamiana muda na tunapendana sana toka shule ya msingi mtamani

Nilimuahidi binti yako sito ugusa mwili wake mpaka siku ya ndoa yetu ama izini yenu wazazi wetu ya sisi kwenda kuishi pamoja

Nilimwacha kijijini baada ya kupata nafasi ya jeshi, Na kumuahidi ni taludi kwa ajili yake na autunze usichana wake.

Maisha yangu sasa ni mazuri na tayari nimeajiliwa na jeshi, nimerudi kutimiza ahadi yangu niliyoiweka nitarudi kwa ajili yake

Baba alichoka baada ya kusikia stori ya mausiano yangu na isaya,na kumuliza.

Ndiyo umerudi kijana wangu lakini umesikia hadithi ya kilicho mkuta mwenzio

Ndio baba nimesikia Isaya alijibu.

"Je ? Bado kweli upo teali kumuoa emerida wangu..?"..... *JE? ITAKUAJE USIKOSE UTAMU HUU .....WA USIO NA KIFANI AKIKA UTOJUTIA KUSOMA NA KURUHUSU KUELIMIKA KUTOKA KWENYE KITABU IKI KILICHO JAAAAAH VISA NA MIKASA KEMKEM INAYO ZUNGUKA KWENYE MAISHA YETU YA KILA SIKU KARIBU KARIBU SANA* .....

KARIBU SANA MPENZI WA SIMULIZI

Edit with WPS Office